

Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo. Accelerating Progress.*

# Ripoti ya Kuongeza Maendeleo
# 2014 - 2016

www.mzfn.org



# *Milele Zanzibar*

Zanzibar ni visiwa vilivyopo kakita Bahari ya Hindi takriban kilomita 30 Mashariki mwa ufukwe wa Tanzania Bara. Zanzibar inashirikisha visiwa viwili vikubwa, Unguja na Pemba, pamoja na vijisiwa vidogo vingi, vingine visivyokaliwa na binaadamu.

Visiwa hivi, ambavyo ni nchi huruinayoendeshwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) iliungana na Tanganyika na kuunda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964. Wakazi wa Zanzibar wamekuwa wakiongezeka kwa kasi, kutoka watu 350,000 hapo mwaka 1967 kufikia milioni 1.3 katika Sensa ya mwaka 2012. Katika Sensa ya mwaka 2015 jumla ya watu ilikisiwa kuwa milioni 1.6.

Ikiwa na urithi mchanganyiko, Zanzibar inajulikana kama "Visiwa vya Marashi", ambapo zamani Zanzibar ilikuwa mwuzaji mkubwa wa viungo duniani. Mabadiliko ya haraka duniani yanayobainisha siasa na uchumi, kushuka kwa bei za mazao, matumizi mabaya pamoja na mapato hafifu kwa serikali, vimeleta mchango hasi kwenye uchumi wa nchi.

Uchumi wa Zanzibar kwa sasa unategemea sana utalii, kilimo na uvuvi, na ingawa uwekezaji katika utalii umekuwa ukiongozeka haraka, hilo halijasaidia kupunguza umasikini. Uchumi wa kilimo na uvuvi umeendelea kuathirika kutokana uzalishaji duni na kwa njia hiyo kutoweza kuchangia ipasavyo uchumi wa nchi kwa ujumla.

Ukijumlisha na ukuaji haraka wa watu hili limeletea kuongezeka kwa hali ya umasikini na kushuka kwa ustawi wa jamii nzima kwa ujumla. Kama sehemu ya Tanzania, Zanzibar haina sifa nzuri katika Vipimo vya Ustawi wa Maendeleo ya Binaadamu vya 2013, ambapo Tanzania imeshika namba 152 kati ya 168 katika kipimo hicho.

Ingawa imeendelea kupanga mikakati ya upunguzaji umasikini, Zanzibar inashindwa kupambana vyema na umasikini ambapo mapato ya asilimia 40 ya watu wake ni chini ya kipimo cha umasikini duniani. Kipimo hiki kinaainisha kuwepo kwa: vifo vingi vya kina mama na watoto wachanga wakati wa kujifungua; wingi wa watoto wenye uzito mdogo na kudumaa kwa watoto wa chini ya miaka mitano; wingi wa vijana wasio na ajira na uzalishaji usio na tija katika kilimo. Sasa Zanzibar inawania kuwa na viwango vya nchi zenye uchumi wa kati itapofikia mwaka 2020 (Dira ya 2020).

Ili kuboresha hali hii, Mfuko wa Milele Zanzibar (Milele Zanzibar Foundation) unashirikiana na wadau katika sekta binafsi, asasi za kijamii na serikali ili kujenga upya miundo-mikakati. Hili litasaidia kupunguza uwiano mbaya katika jamii, kuongeza fursa, upatikanaji wa rasilmali na kukuza maendeleo vijijini.



*Yousuf L. Caires*
*Muasisi wa Shirika na*
*Mkurugenzi Kiongozi wa*
Milele Zanzibar Foundation

Wasiliana nasi kwa:
Instagram, and YouTube:
@MileleZanzibarFoundation

Milele Zanzibar Foundation
*Kuongeza Maendeleo. Accelerating Progress.*

www.mzfn.org

# *Karibu Milele Zanzibar Foundation*

Mpendwa Rafiki wa Milele Zanzibar Foundation, Ikitafsiriwa kutoka "Forever Zanzibar Foundation" Milele Zanzibar Foundation ilianzishwa mwaka 2014 kutokana na jitihada za wapenzi wa Zanzibar duniani kote wenye hamu na ari ya kukuza ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Kwa kushirikiana katika kukabili mapungufu sugu ya maendeleo nchini, na hasa kwa lengo la kuinua hali ya wananchi wahitaji, tumediriki kuchukua hatua za mwanzo na sasa taratibu tumeanza kuona mabadiliko.

Tukitilia mkazo elimu, afya, na uchumi jamii, hasa unaoakisi yale Malengo ya Maendeleo Endelevu Duniani, Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation inashirikiana na wadau mbalimbali kuanzia serikali ya Zanzibar, asasi za kijamii za kitaifa na kimataifa, na kuweza kuchangia katika kukuza miradi ya miundombinu, ya kujenga uwezo na ya kukuza uwezo wa wadau wa maendeleo tunaoshirikiana nao.

Kazi zetu, katika muda huu mfupi wa miaka mitatu, imetoa athari chanya kwa Wazanzibari 200,000 ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya afya, kukarabati na kumalizia madarasa na kujenga shule mpya panapostahiki, kuchapisha vitabu, kuanzisha miradi kwa wanawake na vijana, kilimo endelevu, mafunzo kwa walimu, na uwezeshaji jamii kupitia mikopo kama ripoti hii inavyoonesha.

Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation ina imani na uwezo wa Wazanzibari katika kuinua hali zao za kijamii, kiuchumi na kimazingira, vipimo ambavyo vimeathiri maendeleo.

Walengwa ndio washirika wetu wakuu katika hatua za maendeleo, iwe ni wanajamii wa kijiji cha Bumbwisudi waliotambua mahitaji yao na kuwawezesha kuanzisha kituo cha afya au kumwinua mjasiriamali wa chini kijijini ili kuendeleza ubunifu na uvumbuzi wake wa mashine itumiayo upepo kuzalisha nishati safi na isiyo ghali.

Kwa hiyo, kaulimbiu yaTaasisi ya Milele Zanzibar Foundation, *"Kuongeza Maendeleo: Kunaanzia na Wewe",* kunaakisi uwezo mkubwa ambao tunaamini Wazanzibari wanao katika kujiletea mafanikio endelevu na ya kimtazamo. Dhamira inashabikia nia yetu ya kuleta miradi chanya iliyobuniwa na jamii, ikiainishwa na msaada wetu wa miundombinu, mafunzo na uwezo wa kuiendeleza.

Ili kutimiza dhamira hii tutahakikisha kuwa miradi yetu itaongozwa na maudhui ya kujitolea, ushiriki wa kiraia, *uongozi wa kibinafsi na ubunifu.*

Iwe ni katika kuwawezesha wafanyakazi wa sekta ya afya au vijana wajasiriamali wanaobuni biashara mpya, maadili hayo ndiyo yanayosukuma kukua, maendeleo na mabadiliko.

Milele Zanzibar Foundation ina nia ya kusaidia Zanzibar daima, tukitaraji kuiendeleza mikakati na misaada ya ushirikiano tulioijenga katika miaka mitatu iliyopita katika kukuza na kujenga maendeleo endelevu na ya jumla hapa Visiwani.

Asante Sana na Karibuni.



# Yaliyomo

Karibu Milele Zanzibar Foundation 1

Kuhusu Milele Zanzibar Foundation 4
- Kazi Zetu
- Maono Yetu
- Mtazamo Wetu
- Ushirikiano
- Programu

Programu za Uchumi Jamii 6
- Programu za Uchumi Jamii - Vitengo
- Programu za Uchumi Jamii - Mfano wa Miradi

Programu za Elimu 9
- Programu za Elimu - Vitengo
- Programu za Elimu - Mfano wa Miradi

Programu za Afya 12
Programu za Afya - Mfano

Programu za Miuondo Mbinu 14
Programu za Miuondo Mbinu - Mfano wa Miradi

Mfuko kwa Misaada Midogo 16

Mstakabali Wetu 19

Wafanyakazi wetu 20




# Milele Zanzibar Foundation

**Dira Yetu**
Maono yetu ni kuwa na jumuia mahiri, stahimilivu na za kudumu Unguja na Pemba.

**Dhamira Yetu**
Dhamira yetu ni kuongeza maendeleo katika sekta za afya, elimu na fursa za uchumii jamii vijijini na maeneo ya pembezoni, kupitia programu mahiri na endelevu.

**Mbinu Zetu**
Mbinu za Milele Zanzibar Foundation zinazingatia maendeleo shirikishi yanayoletwa na jamii yenyewe kupitia uwazi unaowawezesha watu binafsi na jumuia nzima kushiriki, kuhamasika, kujijengea uwezo na hatimaye kukabiliana na hali halisi.




## Mfungamano wa Kitaifa na Kimataifa

Mkakati uliopo wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar, (MKUZA III)2016/17-2020/21) unaainisha malengo mengi yanayofungamana na ya Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation yakiwa ni pamoja na:

1. **Maendeleo Endelevu na Shirikishi katika Sekta Muhimu**
2. **Maendeleo ya Rasilmali-watu**
3. **Huduma Kwa Wote**
4. **Kuzingatia Kanuni za Utawala Bora- na**
5. **Maendeleo Endelevu kwa Mazingira**

Jitihada za Taasisi ya MZF zinaungana na za MKUZA III na Mpango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar DIRA 2020 unaolenga kubadilisha uchumi na kuinua maisha ya wananchi kufikia Uchumi wa kati ifikapo 2020. Hii ni pamoja na mikakati ya kimataifa, yakiwemo, Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG), Elimu kwa Wote, na mkazo katika malengo 5 kati ya 17 ya Malengo Endelevu ya Maendeleo, ambayo Serikali ya Zanzibar imeyasaini mwaka 2015.

## United Nation Sustainable Development Goals




## Ushirikiano

*Mashirikiano yanayothaminiwa kati ya Taasisi ya MZF na jamii yanaletea miradi yake kuwa yenye uhalisia, inayoendana na tamaduni na pia kutimiza matakwa na mahitaji ya jamii husika. Asilimia 70 ya mahitaji ya taasisi yananunuliwa toka kwa wananchi na asilimia miamoja ya wafanyakazi wote wasio na ujuzi pia ni wananchi.*

Taasisi ya MZF imeanzishwa kukiwa na imani juu ya mafanikio na maendeleo yanayoshirikisha jumuia ya watu wenye mtazamo mmoja ulio makini, na wakawa na muono yakinifu. Kushirikiana na kujenga mahusiano mema ni muhimu katika kutimiza wajibu na harakati za Taasisi ya MZF na malengo yake.


Kwa hiyo, Taasisi ya MZF inajenga mahusiano thabiti na serikali, katika jumuia na hata na katika asasi za kijamii na sekta binafsi. Mashirikiano hayo yamewezesha taasisi kuwa na miradi yenye maudhui bora, yanayoeleweka, yanayolingana na mikakati na sera za kitaifa, na hatimaye ni miradi inayoweza kuainishika na kuwa endelevu. Mahusiano yetu na jamii yameweza kuwafikia viongozi wa jumuia mbalimbali, wajasiriamali, mafundi na wafanya biashara na hivyo kutuwezesha kuwasaidia kwa uhakika wale wasio na uwezo, na kudhamini mikakati ya maendeleo katika jamii.


## PROGRAMU

TAASISI YA MILELE ZANZIBAR FOUNDATION imeainisha mpango-mkakati ulio wazi na unaozingatia maswala muhimu ya afya, elimu na fursa za uchumi jamii vijijini na kwenye maeneo yasiyofikika kwa urahisi kupitia program za maendeleo endelevu. Miundombinu, usawa wa kijinsia, ufanisi wa nishati, maji na usafi wa mazingira pamoja na udumishaji wake, vinaendelea kuwa mambo yanayozingatiwa katika miradi yote na katika sekta zote tatu. Wakati mwaka 2014 ulikuwa mwaka wa kujenga misingi, katika mwaka 2015 tulizingatia kuendeleza na kukuza mashirikiano.

Katika mwaka 2016 kiwango cha mipango ya Taasisi ya MZF ilikua hadi kuifikia miradi 15 inayowagusa watu takriban 200,000, katika vijiji 50 vya Unguja na Pemba.

## Hatua za maendeleo zilizofikiwa hadi sasa




**Kuongezeka kwa Upatikanaji wa huduma bora za Afya vijijini**

Wanawake 1,906 wapo karibu na huduma ya afya ya uzazi kabla na baada ya kujifungua. Ndani ya miezi 4 kunaongezeko la 69% kwa kina mama kuhudhuria kituo cha afaya kabla na baada ya kujifungua.

Wanaume, wanawake na watoto wapatao 26,790,wanafurahia upatikanaji wa kituo kipya cha Afya cha jamaii na msaada wa ziada kwa ajili ya afya ya uzazi

Vituo vya Afya vya Umma vimepatiwa vitanda 48 vipya

Vinara wa Afya 47 wamejitolea kutumikia katika vituo vya afya vya vijijini

**15,000** Mabomba na mahodhi ya kuhifadhia maji yamejengwa ili kuwanufaisha wanavijiji wa Makunduchi na kisiwa cha Uzi




## KUONGEZA KIPATO CHA FAMILIA

Zanzibar ni nchi changa na tegemezi. Kama ilivyo katika nchi zinazoendelea, mwajiri mkubwa ni serikali, wakati sekta binafsi inaendelea kudumaa. Waishio vijijini wanajishughulisha zaidi na kilimo cha jembe, uvuvi na ufugaji duni ili kujikimu kimaisha. Kwa sababu hiyo asilimia 30.4 ya Wazanzibari, hususani vijana na wanawake, wana kipato ambacho ni chini ya kipimo cha umasikini.

Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation, kupitia program ya Uchumi Jamii, ina nia ya kuwawezesha vijana na wanawake vijijini kupitia miradi ya uzalishaji mali, Kuwaongezea ujuzi wa kitaalamu wa kushajihisha imani ya kujitegemea, kuwa na uwezo endelevu wa kukabiliana na hali halisi. Katika miaka ya 2015-2016 sekta ya Uchumi Jamii ilitekeleza miradi kadha iliyosaidia kuongeza kipato na na kuweza kuinua hali ya maisha ya zaidi ya watu 10,000.

# KITENGO CHA UCHUMI JAMII

## 1) Fursa za Kiuchumi Kwa Wanawake na watu wenye Mahitaji Maalum

### Uwezeshaji wa Wanawake Zanzibar (WEZAII)

***Mshirika:*** Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania- (TAMWA)
***Wanaofaidika***: Wanawake 7,000 na vyama 350 vya Kuweka na Kukopa (VIKOBA)
***Maelezo:*** Mradi huu unalenga kupunguza umasikini na kuleta usawa kwa jamii za Kizanzibari kwa kusaidia wanawake 7000 wa vijijini kutoka wilaya 8 za Unguja na Pemba na kuongeza kipato na pia kupunguza vizuizi vya kijamii, kitamaduni na vya kisiasa katika kujipa uwezo.

### Mradi wa nishati ya jua Zanzibar

***Mshirika:*** Barefoot College
***Wanaofaidika:*** Kaya 450 na watu 2700 katika vijiji 4.
***Maelezo:*** Mradi unalenga kuinua ubora wa maisha ya wanajamii waishio vijijini na maeneo ya pembezoni kwa kuwawezesha kupata nishati ya jua ilio safi na salama kwa afya, na kuongeza kipato na fursa za kiuchumi kwa sola mama na kuongeza uwekaji hakiba kwa kaya za vijijini.

### Msaada wa Maendeleo ya Kongano Bunifu La Mwani Zanzibar

***Mshirika:*** Zanzibar Seaweed Cluster (Kongano Bunifu la Mwani Zanzibar)
***Wanaofaidika:*** Wanawake 500/wanaume 300;
Shehia 16. ***Maelezo:*** Mradi unalenga kukuza na kupanua uzalishaji na kipato kwa sekta ya mwani kwa kuongeza uratibu, upataji wa taarifa na kukuza elimu kwa wakulima wa mwani hususan wanawake.

## 2) Vijana na Ujasiriamali

### Mradi wa Fursa Kijani-/Vijana, Ajira na Maendeleo endelevu

***Washirika:*** Practical Permaculture Institute of Zanzibar (PPIZ); Fumba Town Service Center (FTSC);
Volunteer Services Overseas (VSO);
***Wanaofaidika:*** Vijana 60 walioacha shule kutoka wilaya 11 za Unguja na Pemba.
***Maelezo:*** Kushajihisha utunzaji wa mazingira kupitia kilimo salama chenyekutumia mbolea asilia, kujenga na kuendeleza taratibu za kiuchumi.

### Mfuko Endelevu wa MZF/ZTBI

***Mshiriki:*** Zanzibar Technology and Business Incubation (ZTBI)
***Wanaofaidika:*** Watu 530 (wake 454 na waume 76) Vikundi 40. ***Maelezo:*** idadi ya wajasiriamali vijana waliofanikiwa kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia mtaji wa kuanzisha biashara zao kupitia Mfuko endelevu

## 3) Kilimo cha Mboga na Matunda, Biashara ya Kilimo na Upatikanaji wa Masoko

### Kujenga uwezo wa Wakulima wa Kilimo wa mbogamboga.

***Washirika:*** Tanzania Horticultural Association (TAHA) (Jumuiya ya Wakulima wa Mboga na Matunda Tanzania).
***Wanaofaidika:*** 614 (Wake143/waume471); Mashamba 20 yaliopatiwa mashine ya kuvutia maji inayotumia nishati ya jua.
***Maelezo:*** Mradi unalenga kuongeza uzalishaji kwa wakulima wadogo wadogo wa mboga mboga na kuongeza kipato chao kwa kuwapa ruzuku ya 50% ya bei za pembejeo na kuwawekea mashine ya kuvutia maji kwa wakulima wanachama wa TAHA.





# MFANO HAI WA PROGRAMU ZA UCHUMI JAMII

## Kujenga uwezo wa Wakulima wa mboga na matunda

Ikishirikiana na Chama cha wakulima wa mboga  na matunda(TAHA), Milele Zazibar inawapa wakulima waliopata mafunzo, pembejeo za lazima kama maji, mabomba ya umwagiliaji, mbegu, mbolea, na vifaa muhimu vya kilimo zitazosaidia kuwaongezea wakulima kujiamini na kuweza kuzalisha mazao bora zaidi. Mwaka huu, hii imesaidia kuongeza uzalishaji, kipato na akiba. Wakulima wameweza kujiwekea akiba yenye thamani ya Shilingi 225,096,475 ili kuongeza uzalishaji kwa kununua vifaa, mbolea na dawa za wadudu wakipatiwa ruzuku ya 50% ya bei kutoka Taasisi ya MZF. Nchi imeonekana kuweza kupunguza uagizaji wa mazao ya Kilimo-mboga na matunda kutoka Tanzania Bara.  Uagizaji ulikuwa 80% mwaka 2010 na 20% mwaka 2016 na kuiingizia nchi Dola za Kimarekani milioni 39 (RGoZ).

Kutokana na hilo wakulima wa tungule wa TAHA wamejikuta wana ongezeko la pato kwa kiwango cha 115% mwaka 2016 ukipimia na mapato ya mwaka 2015.

### WAKULIMA WA KILIMO MBOGA NA MATUNDA

► Wakulima 614 (471wake/143waume) waliofundishwa mbinu za ukulima bora Unguja: 283 waume and 76 Wake. Pemba: 188 waume and 67 wake walipatiwa ruzuku ya 50%

► Maeneo manne, yaliyoko Unguja na Pemba yamewezeshwa kuwa na mashine ya kuvutia maji inayotumia nishati ya jua.

► Kumekuwa na muongezeka kwa mahusiano kati ya wakulima na masoko ya ndani na  ya nje.



## MABADILIKO YA KIUCHUMI – Uwezeshaji wa Wanawake zanzibar

*Bi. Batuli Ali Omar*

Bi Batuli Ali Omar ni mama wa watoto sita anayekaa Mfikiwa, Chake Chake, Pemba anayeshiriki katika mradi wa Uwezeshaji wa Wanawake Zanzibar II (WEZA II). Mradi wa WEZA II unajitihada za kuwawezesha na kuwasaidia wanawake wa Unguja na Pemba ili kupunguza umasikini Zanzibar na kuendeleza Haki za Jamii.
Kutokana na mumewe kupata ugonjwa wa kupooza Bi Batuli ndiye pekee mtafutaji wa kipato cha familia. Baada ya kuanzishwa kwa WEZA II kwa ushirikiano na TAMWA, Bi Batuli alijiunga na Chama cha Kuweka na Kukopa, Allah Tuwezeshe, huko Mfikiwa, Pemba. Kikundi kina wanachama 15 na kina kusanya jumla ya Shilingi 2500 kila wiki toka kwa kila mwanachama. Kutokana na kujituma kwake binafsi na kundi zima kwa miezi mitatu Bi Batuli aliweza kupewa mkopo wa Shilingi 150,000 ili kuanza mradi wa maendeleo. Akiongeza shilingi 70,000 zake mwenyewe alianzisha mradi wa kuuza mkaa kwa jumla.

Mtaji wake umekua hata kufikia Shilingi 400,000 katika miezi mitatu na kumwezesha Bi Batuli  kununua magunia 35 ya mkaa. Bi Batuli ameweza kuongeza jitihada na kuanzisha mradi mwingine wa kujiongezea kipato kwa kulima mboga.
Sasa Bi Batuli anaweza kujikimu kimaisha, kulipa ada za shule, kununua vitabu, kalamu na sare za shule kwa watoto wake watano waendao shule. Bi Batuli ana mpango wa kuanzisha mradi wa biashara ya nazi akitumia faida ilotokana na biashara ya mkaa ambayo ana mpango wa kuipanua.

## KUONGEZA UPATIKANAJI WA ELIMU SALAMA NA BORA


Tukifuatilia takwimu za elimu Zanzibar, zinajionesha kuwa hivi sasa watoto wengi, wasichana kwa wavulana wanakwenda shule: jumla ya 84% ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule wameandikishwa.

Licha ya kuongezeka kwa uwelewa wa umuhimu wa kwenda shule , inakadiriwa kuwa jumla ya watoto wa umri wa shule wapatao 69,000 bado hawaendi shule Zanzibar. Na hao wanaokwenda shule bado si waelewa katika kusoma na kuandika na hatimaye 20% hawafaulu mtihani wa darasa la saba. Mwishoe takriban 50% ya wanafunzi wanaacha shule kwa sababu ya kutofaulu mitihani yao ya kidatu cha 2.

Kuna wingi wa sababu zikiwemo madarasa machache na yanayofurika wanafunzi, walimu wasio na utaalamu na wasiolipwa vizuri, pamoja na uhaba wa vifaa vya kufundishia. Sababu zote hizi zinaletea kuwa na matokeo mabaya. Mikakati ya Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation inayozingatia kushirikiana na wadau wa elimu inalenga kujibu changamoto hizo kwa njia zifuatazo:

1) **Kuwezesha uwepo wa mazingira salama ya kusomea na yaliyo mazuri.**
2) **Kukuza ufundishaji bora na unaokimu matakwa ya elimu kwa karne ya 21 toka chekechea hadi vyuoni.**

Katika muhula wa 2015 -2016 programu za Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation ziliweza kusaidia skuli 60 kwa kuchukua hatua kadha zinazohusisha miundombinu, udhamini, mafunzo na program za kujenga uwezo zilizowagusa wanafunzi na walimu 200,000.



# ELIMU

# PROGRAMU ZA ELIMU- VITENGO

## 1) Upatikanaji wa mazingira salama na mazuri kwa kujifunzia.

**a.) Skuli Yetu ni Hazina Yetu**
***Mshirika:*** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
***Wanaofaidika:*** Wanafunzi 7,338 (3,591waume/3,747 wake); Skuli 13
***Maelezo***: Mradi huu unalenga kuongeza uandikishaji na mahudhurio kwa wanafunzi wa chekechea, shule za msingi na sekondari kwa kutengeneza mazingira bora na kwa kumalizia ujenzi wa madarasa, vyoo na nyumba za walimu.

**b) Mradi wa ukarabati wa mapaa ya Skuli**
***Mshirika:*** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
***Wanaofaidika:*** 25,056 (12,474 wake/12,582 waume); Skuli 39
***Maelezo:*** Mradi huu unalenga kuboresha mahudhurio na mazingira ya kusomea kwa wanafunzi hasa wakati wa mvua, kwa kupunguza wingi wa madarasa hatarishi kote Unguja na Pemba

## 2) Kukuza Ubora wa Mafunzo na Matokeo yake:

**a) Milele Elimu Zanzibar (MEZA II)**
***b) Mshirika:*** Jukwaa la Wanawake Wasomi Waafrika, Zanzibar (FAWE Zanzibar)
***Wanaofaidika:*** Wanafunzi 450 (263wake/87waume); Skuli 30
***Maelezo:*** Mradi huu unalenga kuboresha mvuto na utendaji wa wanafunzi, hasa wasichana, katika masomo ya STEM, kwa kuwapatia udhamini, ujuzi wa maisha na uwezeshwaji kuhusu uongozi kupitia vikundi vya TUSEME na STEM katika mashule ya sekondari.

**c) Kukuza lugha ya Kiingereza na kusoma na kuandika**
***Mshirika:*** Taasisi ya Elimu Zanzibar
***Wanaofaidika:*** Wanafunzi 200,000 wa Darasa 1 hadi 4; Walimu wa Kiingereza 1,600.
***Maelezo:*** Mradi huu unalenga kuboresha utendaji wa wanafunzi katika skuli za msingi na kuongeza uwezo wa walimu wa lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili na uwezo wa wanafunzi wa kusoma na kuandika kwa ujumla ili kukidhi kiwango kinachotarajiwa, na upatikanaji wa vitabu vya Kiingereza na vitabu elekezi vya walimu.

# PROGRAMU ZA MFANO ZA ELIMU




## Skuli Yetu ni Hazina Yetu (SYNHY)

Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation imeshirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (MOEVT) ili kukamilisha ujenzi na ukarabati wa madarasa katika skuli 21 Unguja na Pemba ili kuboresha mazingira ya kujifundishia, katika miaka mitatu. Ikitimiza lengo lao la kuongeza kasi ya maendeleo kwa kutumia mikakati kamilifu na endelevu, Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation kupitia program ya Skuli Yetu ni Hazina Yetu (SYNHY), imeweza kumalizia madarasa yalioanza kushughulikiwa na jamii husika napia imehakikisha kuwa kila skuli inawezeshwa kupata maji, vyoo na umeme kama haupo.

Mpango huu wenye shughuli za kina, zikiunganishwa na ujenzi wa nyumba za walimu katika skuli za vijijini, unalenga kukuza uandikishwaji wa wanafunzi, kuboresha mahudhurio ya wanafunzi na walimu, ili kuendeleza ubora wa ufundishaji na matokeo na hata kusikia furaha katika kujifunza.

# MFANO HAI WA PROGRAMU ZAELIMU




**Skuli Yetu ni Hazina Yetu (SYNHY)- MATOKEO YA MDA**

- Kuongezeka kwa uandikishaji katika baadhi ya shule zetu
- Kuboresha mahudhurio katika maskuli
- Kuboresha mahudhurio ya walimu katika maskuli maalum

**Skuli Yetu ni Hazina Yetu (SYNHY) MATOKEO YA MDA MFUPI**

- Wanafunzi 7,338 (3,591 waume/ 3,747 wake) walifaidika
- Walimu 24 wamehitimu mafunzo na kuelewa utaratibu bora wa usafi na afya
- Kumalizia / ukarabati wa madarasa 49,ofisi pamoja na kujenga skuli 2 mapya
- Ujenzi na ukarabati wa vyoo 108
- Ujenzi wa nyumba za walimu 5
- Ujenzi wa ofisi 6
- Uchimbaji wa Visima 4 na matangi ya maji 7
- Walimu 24 walifunzwa ujuzi wa usafi wa SWASH
- Upatikanaji wa madawati 350
- Jamii ilifaidika kutokana na uwepo wa maji maskulini hapo Mkanyageni, Bandamaji na Mbuyutende.




## Vitabu na Mafunzo ya Kujua Kusoma na Kuandika Kingereza

Katika jitihada za kuboresha uelewa wa lugha ya Kiingereza kusoma na kuandika, Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation iliandaa na kuchapisha vitabu "Tujifunze: Kiingereza kwa Skuli za Zanzibar" kwa ajili ya darasa 1 hadi 4 vilivyochapishwa na Oxford University Press.

Vitabu hivi ni vya aina yake na vimelengwa kufundishia wanafunzi Zanzibar, vikiheshimu na kuzingatia mila na utamaduni katika michoro na mpangilio wa kitabu na mafunzo yenyewe. Uchapaji wa vitabu hivi kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni sehemu ya utashi wa Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation katika kuboresha upatikanaji na utoaji wa elimu bora Zanzibar, kwa kudhibiti misingi ya uelewa na usomaji Kiingereza, lugha ambayo inakuwa lugha ya kufundishia kuanzia darasa la 5.

Vitabu hivyo vinaambatana na Muongozo wa Mwalimu kwa kila darasa ili kuhakikisha uelewa na kuongeza uwezo wa mwalimu anayefundisha Kiingereza kama lugha ya pili. Vitabu vya Wanafunzi na Muongozo wa Mwalimu vilihakikiwa na wataalamu wa lugha ya Kiingereza wenyeji ili kuhakikisha ubora.

Mafunzo elekezi yalitolewa kwa walimu wa Kiingereza wapatao 1600 kwa kutumia Walimu wa Walimu 75 wakikazia ujuzi unaohitajika kutumia vitabu, kuonyesha njia zitakazowawezesha walimu kushirikisha wanafunzi katika kutumia vitendea kazi. Hii pia inabainisha uelewa na utumiaji wa kiingereza kwa walimu.

*Vitabu 200,000 vya "Tujifunze: Kiingereza kwa Skuli za Msingi za Zanzibar" vilifikishwa kwenye skuli za Zanzibar mwezi Februari 2017.to Zanzibar classrooms in February 2017.*




## KUPANUA UPATIKANAJI WA AFYA BORA VIJIJINI

Mipango ya Afya ya Milele Zanzibar Foundation imelenga upatikanaji wa huduma bora za Afya ili kupunguza kasi ya vifo vya watoto wachanga na wajawazito.

Kwa kuwepo Vituo vya Afya karibu 80 nchini, sekta ya Afya Zanzibar imeweza kupunguza umbali wa kufikia kituo cha afya hadi kilomita 5.
Hata hivyo Zanzibar bado inahangaikia kupunguza vifo vinavyokingika ikiwa ni pamoja na kasi ya vifo vya watoto wachanga na kina mama wajawazito vinavyobainishwa kuwa ni 46/1000 na 310/100,000.

Sababu zinazochangia kuwa na huduma mbaya ya afya kwa mama na mtoto ni pamoja na kuchelewa kwenda kituoni kwa huduma za uzazi. Hii inatokana na ufahamu mdogo wa umuhimu wa huduma za uzazi, uchelewaji wa kupata huduma hizo na huduma mbovu kutokana na kukosa vifaa, madawa, wahudumu wenye utaalamu na waliofunzwa vyema.

# KUPANUA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA AFYA VIJIJINI

## Afya Ya Mama Ni Maendeleo Kwa Taifa (Mother's Health Is Nation's Progress)

Mkakati wa awali wa Milele Zanzibar Foundation wa kukabiliana na masuala ya afya Zanzibar, hususan afya ya uzazi, umelenga kuendeleza na kuboresha miundo iliopo ili kuwawezesha kinamama kufikia na kupata huduma bora za afya katika vituo vizuri na vya kisasa.

Tukishirikiana kwa ukaribu na Wizara ya Afya katika mradi wa "Afya ya Mama ni Maendeleo kwa Taifa", mradi umelenga kumalizia ujenzi na kukarabati vituo 27 vya afya vilivyopo katika vijiji vya Unguja na Pemba. Vituo vinane vilivyoko mijiji na vijijini, na hata makazi yenye watu wengi yaliyoko Unguja na Pemba, wamejengewa vituo vya afya pamoja na wodi za wagonjwa, vyoo, nyumba za wafanyakazi na upatikanaji mzuri wa maji safi na salama. Maelfu ya wanajamii hizo, hasa wanawake waja wazito na watoto chini ya miaka mitano, sasa wanafurahia upatikanaji wa huduma bora safi na salama za afya vijijini mwao.

## Wafanyakazi wa Huduma za Afya Katika Jamii: Kustawisha Afya Bora Vijijini

Program ya "Vinara Katika Afya" unaunga mkono upatikanaji, na utoaji wa huduma za afya vijijini. Progamu hio inawadhamini wanafunzi wasiojiweza kifedha, nawanaofaulu vizuri (wanafunzi hodari), wanaotokea vijijini Zanzibar kusoma katika Chuo cha Sayansi za Afya Zanzibar, wakiwa na ahadi ya kurudi vijijini walikotokea(au kijiji chochote kile) baada ya masomo yao, na kufanya kazi japo kwa miaka miwili. Udhamini huo, ukoiambatana na program za utoaji wa masomo ya taaluma husika, ushauri na kujitolea umeweza kuwahamasisha wanafunzi kuzidi kuwania na kupenda kufanya kazi katika huduma za afya hasa vijijini.

Jecha na Mulhat, waliomo katika picha hapa, hivi karibuni watahitimu na kurudi Pemba ambako tayari wameweza kushiriki kufundisha na kueneza elimu ya Afya kwa wanavijiji kuhusu kipindupindu, maji hatarishi, magonjwa ya watoto chini ya umri wa miaka 5 na shindikizo la damu. Vinara 47 wameshajitolea katika vituo kadha mwaka 2016.












# PROGRAMU ZA MIUNDO MBINU



Vifaa vingi vilivyoko Zanzibar ni vikongwe na havitunzwi vyema hasa katika vijiji na sehemu zisizofikika kwa urahisi, na hivyo kuchangia katika kuwepo kwa upungufu wa huduma za maji safi na salama, nishati safi, barabara na nyumba. Maendeleo ya haraka yataweza kupatikana iwapo vikwazo hivi vitashughulikiwa. Japokuwa uimarishaji wa miundombinu ni moja kati ya mikakati ya Taasisi ya MZF, hasa katika sekta za Elimu, Afya, na Uchumi Jamii, Taasisi pia inasimamia miradi mikubwa ya miundombinu.

## Mfano hai wa Mradi

Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation imeanzisha ujengaji wa minara mikubwa ya usambazaji maji kwa ajili ya vijiji vya Uzi na Makunduchi.

Miradi hii miwili inatarajiwa kuwafikishia maji zaidi ya watu 15,000 na kuwawezesha kupata maji safi.

Mradi wa Maji Makunduchi ni mradi wa uwekezaji wa mabilioni ya fedha ili kujenga bomba la maji, kuweka pampu, kusafirisha maji na kukarabati minara ya maji ili kufikisha maji safi kiasi cha kilometa 3 hadi kufikia vijiji vya Makunduchi na Kibuteni.



# MFUKO WA MISAADA MIDOGO

Mradi wa misaada midogo wa Milele Zanzibar Foundation wa mwaka 2016 umewawanufaisha zaidi ya watu 10,000 ulitoa misaada kwa jamii katika visiwa vya Unguja na Pemba. Misaada ya Haraka imeiwezesha taasisi ya MZF kupanua ufikiaji wake kwa jamii zenye mahitaji, ambapo ni vigumu kuzifikia jamii ambazo hazinufaiki na miradi mingineya MZF au program nyingine. Watu binafsi na taasisi wameweza kuomba na kupata msaada wa fedha hadi  shilingi milioni 20.

Kwa njia hiyo, Mradi wa Misaada midogo imesaidia miradi 15 katika sekta kuu MZF Elimu, Afya na Uchumi jamii na kuongezeza sekta moja nyingine,Dharura. ambayo ilipewa nafasi maalum kwa sababu ya majanga kadhaa yaliyoikumba Zanzibar mwaka 2016, ikiwa ni pamoja na mafuriko, mripuko wa kipindupindu na moto. Katika mwaka wa mwanzo tu MZF ilipitia jumla ya  maombi 269 kutoka kwa jumuiya za Unguja na Pemba. Miradi 12 kutoka Unguja yalichaguliwa na miradi mitatu kutoka Pemba.



## Mfuko wa Misaada Midogo

### Katika Elimu: wanafunzi 522

- Usambazaji wa vifaa mashuleni ikiwa pamoja na vifaa vya kufundishia, na kompyuta.
- Misaada maalum kwa Wanafunzi Wasiojiweza na Walimu
- Ukarabatishaji, umaliziaji na utoaji vifaa kwenye vituo vya elimu ya dini (Madrasa)

### Katika Afya: Wagonjwa2,045

- Vifaa vya Utoaji Afya na Madawa
- Kusaidia Wagonjwa wenye upungufu wa akili
- Kusaidia Mazingira na Usafi (hasa vifaa vya usafi) katika vituo vya afya







### Katika Uchumi Jamii: Wanavijiji 7776

- Uchimbaji wa visima na upatikanaji wa maji safi na salama
- Usambazaji wa nishati ya Jua, na uwepo wa nishati endelevu
- Ujenzi wa karakana kwa ufundishaji na utayarishaji wa Mwani na kuuongezea thamani
- Miundombinu (barabara na madaraja

### Msaada kwa Dharura:

- Moto
- Mlipuko wa Kipindupindu
- Mvua kali, Mafuriko na upepo wa kimbunga
- Njaa na Ukame
- Waathirika wa Ajali

## MRADI WA MFANO

### Msaada wa Dharura kwa Majanga

Mwezi Machi 2016 Zanzibar ilikumbwa na janga la mlipuko wa kipindupindu. Iliripotiwa kuwa Zanzibar ilikuwa na wagonjwa wa kipindupindu 3000 na kusababisha vifo vya watu 51, kutoka Mikoa mitano.

Vifo vingi zaidi vilitokea Unguja (Wagonjwa 1818 na vifo 38) wakati Pemba wakiripoti wagonjwa 1239 na vifo 13.

Sababu kuu zilizochangia kusambaa kwa ugonjwa Tanzania Bara na Zanzibar ilikuwa ni ukosekanaji wa maji safi na uchafu wa mazingira uliokithiri.

MZF iliweza kuitikia haraka kwa kutoa Msaada wa Dharura ili kuwezesha kupatikana kwa vifaa na madawa.

Dawa, mafuta kwa usafiri, vyombo vya kusafishia na vifaa vingine vilipelekwa kwenye kituo cha Kipindupindu Chumbuni, Unguja Magharibi, ili kusaidia kutibu na kuzuia ongezeko la ugonjwa.


1kg

# Mtazamo wa Mbele

Katika kujenga na kuimarisha uwezo wetu na kazi zilizofanywa hadi sasa Milele Zanzibar Foundation imeweka mikakati maalumu kwa miaka mitatu ijayo ya utekelezaji wa programu kwa kuzingatia maeneo muhimu ya matokeo mazuri kwa kutumia mifano chanya ya uwezeshaji inayotokana na mtazamo wa maendeleo ya kijumla kama:

**Kuimarisha utaalamu wa kiufundi, ustadi na taaluma katika utoaji wa huduma hasa kwa walimu.**

**Kuwezesha vijana kwa kupitia mbinu za uongozi na ubunifu katika ujasiriamali na uzalishaji wenye tija katika sekta muhimu za uchumi.**

**Kuimarisha mifumo na kukuza ushirikishwaji katika sekta nzima, kupanua na kuimarisha uwezo wa ushirikiano na wadau wengine.**

## *Inaanza na Wewe!*

Dhamira kuu ya Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation kwa mwaka 2017 ni: "Kuongeza Maendeleo: Kunaanzia na Wewe". Dhamira hii mpya na pana inafafanua kazi na mtazamo wa kipekee wa Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation Hizi ni kazi zinazoendelezwa na jumuia husika ili kukuza kujitegemea na kujijengea uwezo na kuleta maendeleo yaliyo endelevu.

"Kuharakisha Maendeleo: Wa mwanzo Ni Wewe", inatilia mkazo mtazamo wa kitaasisi kuwa watu binafsi ndio waleta mabadiliko, na kwa mvuto wao wanao uwezo wa kuleta mabadiliko ili kupunguza umasikini Zanzibar.

Kazi inayosimamiwa na Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation ambayo inaendeleza juhudi za wanajamii, imeweza kufanikiwa kutokana na mfumo wa mashirikiano na uwezeshaji wa taasisi na inaonesha jinsi Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation ilivyo katika nafasi maalum ili kusukuma nia yake ya kuiwezesha jamii kupitia mikakati yake inayokazia elimu, afya na uchumi jamii.

**Tufuatilie kupitia:** @milelezanzibarfoundation

Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo. Accelerating Progress.*

# Wafanyakazi Wetu

**Yousuf L. Caires**
*Muasisi Shirika na Mkurugenzi Kiongozi*

**Kassim Mbarouk Juma**
*Mkuu wa Uendeshaji*

**Khamis Rashid Khalfan**
*Mhandisi wa Miradi- Unguja*

**Zariha Haji Abasi**
*Afisa Utawala- Unguja*

**Ali Mohamed Mbarouk**
*Mhasibu*

**Hassan Ubwa**
*Afisa Manunuzi*

**Abdillah Yahya Hassan**
*Usafiri*

**Faida Kassim**
*Mhudumu- Unguja*

**Mshauri Hassan**
*Mhudumu - Pemba*

**Mohammed Shehe**
*Mhandisi wa Miradi - Pemba*

**Khadija Ahmed Shariff**
*Mkuu wa Programu*

**Ali Bakari Amani**
*Mratibu wa Miradi- Elimu*

**Alice Macmilian Mushi**
*Mratibu wa Miradi- Uchumi Jamii*

**Eshe Haji Ramadhani**
*Afisa Miradi- Unguja*

**Abdallah Said Abdallah**
*Mkuu wa Ofisi-Pemba*

**Fatma Khamis Silima**
*Afisa Miradi-Pemba*

**Said Mzee**
*Usafiri - Pemba*

**Asha Seif**
*Afisa Utawala- Pemba*

**Zuhirah Khaldun-Diarra**
*Mtaalamu wa Mawasiliano*



**Kwa maelezo zaidi tufuatilie kupitia**
www.mzfn.org
@milelezanzibarfoundation

Milele Zanzibar Foundation

*Kuongeza Maendeleo. Accelerating Progress.*



Milele Zanzibar Foundation
Mbweni, P.O. BOX 933, Zanzibar
Tel: +255772229997, Email: info@mzfn.org
www.mzfn.org

@milelezanzibarfoundation